# ANDIKO LA DHANA YA UTEKELEZAJI

# WA KAMPENI YA ‘SAFISHA

# PENDEZESHA WILAYA YA KATI’

# BARAZA LA MJI KATI

# 2025 - 2026

## UTANGULIZI

Kampeni ya "Safisha na Pendezesha Wilaya ya Kati" inalenga kuimarisha usafi wa mazingira, kupendezesha maeneo ya wazi, kuhimiza matumizi ya nishati safi, na kuongeza ushiriki wa jamii katika kulinda, kusafisha, kun'garisha na kupendezesha mazingira. Hii ni katika sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Miradi Zanzibar, hasa kupitia Mkakati wa Mazingira na Maafa Zanzibar, ambao kwa Baraza la Mji Kati itatekeleza kampeni hii kwa kuongozwa na kufuata vipengele vya kimkakati katika upendezeshaji na Ung'arishaji wa Miji kama vifuatavyo:

***Kuanzisha jadi za kijani (green corridors & open spaces)***

Kupitia Historic Urban Landscape Atlas, mpango huu unasisitiza ujenzi wa green corridors katika maeneo ya umma yenye miti na viwanja vya wazi ili kupunguza tatizo la umaskini wa anga yaani uwenevu wa hewa ya $CO_2$, ikizingatiwa Wilaya ya Kati kwa kisiwa cha Unguja ndio yenye eneo kubwa la ukijani, hivyo katika maeneo ya barabara kuu yenye kijani kibichi na uoto wenye kuvutia yanayofaa ni kama vile Dunga (Dunga zuze, Mwera Pongwe, Kidimni – Kitope, Bango la Mkoa – Tunguu, kwa upande wa njia za ndani ni Jumbi, Dunga – Bambi, Umbuji -Mchangani). Hizi ni sehemu zenye kuunganisha maeneo ya kihistoria na makazi mapya ambazo kuboroshwa kwake kutaongeza mandhari zenye vitalu vya kuvutia na bustani za kijani zitakazopendeza zaidi.

***Kuimarisha miundo mbinu ya kijani (eco-infrastructure)***

Kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Mazingira, Programu ya **Green and Smart Cities** iliyozinduliwa huko Pemba (vile vile inayofadhili uwekezaji Pemba/Tanga/Mwanza) inalenga kukuza green infrastructure kama mifereji ya maji, usafishaji taka na miundombinu inayozingatia upangaji wa maji, kupunguza kupanda kwa kupanda joto, na kuboresha mazingira ya mji kwa ujumla. Hivyo kwa upande wa Baraza la Mji Kati kupitia utekelezaji wa kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha uchakataji wa taka, litaandaa iundombinu ya maji kwa jamii ikiwemo mifereji katika vituo vya daladala, vyoo na bustani kupitia mapato yake au muwekezaji atakaefadhili kampeni hii.

***Usafi wa mazingira na usimamizi wa taka***

Sera ya Mazingira ya Zanzibar (2013) inaeleza haki ya kuendeleza mfumo madhubuti wa usimamizi wa taka na uchafuzi, ikiwa ni pamoja na elimu ya umma na viwango vya ubora wa mazingira, kusaidia kupunguza uchafuzi uliopo mijini/Shehiani.

Baraza la Mji Kati pamoja na kutumia viwango vya taifa au kimataifa hata hivyo Baraza litaweka viwango vya usafi wa kila eneo, vitakavyotumika kwa ajili ya kumpata mshindi katika maeneo ya Shehia, maduka, vioski, viwanda, maskuli, na hospitali, mazingira ya biashara mengineyo, njia na vyuo sambamba na aina za haiba zitakazokuwepo ndani ya

Wilaya ya Kati kama vile Sanamu za Kima punju, Vinu na michi, Pomboo na Mabango ya Kisasa.

***Kugundua na kulinda mandhari za kihistoria***

Katika Zanzibar City Centre Local Area Plan, mpango unasisitiza ulinzi wa mandhari ya kihistoria, utunzaji wa mazingira, na miundombinu rafiki kwa watembea kwa miguu, kuhakikisha mji unakuwa salama, mzuri, mazingira rafiki na kivutio cha utalii. Hivyo kupitia kampeni hii itatekeleza mkakati huo kwa kuweka vivutio vya vinyago vitakavyoweza kutoa taaswira ya tunu zilizomo ndani ya Baraza la Mji Kati kama vile Pomboo, Kimapunju na Vinu na michi, mabango ya kidigitali.

***Kuongeza maeneo ya kijani kwa upandaji miti makini***

Mradi wa TUI Forest Zanzibar umepunguza vikwazo vya kijani pamoja na uimarishaji wa mijini kwa upandaji miti 63,000 karibu na maeneo ya Stone Town ili kuzuia jangwa na kurejesha mazingira safi. Hivyo kwa Baraza la Mji Kati litafanya kazi hiyo pamoja na wadau tajwa kwa kufadhili kupatikanwa kwa miti sambamba na kushiriki kuipanda miti yote kabla muda wa utekelezaji wa kampeni hii haujamalizika.

***Uwekezaji na msaada wa kitaifa na kimataifa***

Zanzibar inafaidika na ruzuku na msaada wa kimataifa kama €1.2 milioni kwa msaada wa mipango ya maji taka, usafishaji, upendezashaji, usafiri mbadala na uwekaji maeneo ya kijani katika Stone Town, na Mpango wa Taifa wa Nishati Safi Tanzania.

Hivyo kwa Unguja Wilaya ya Kati ndio yenye eneo mahsusi la uwekezaji katika viwanda ikiwa ndio eneo lilijengwa kiwanda cha Atomic Nuclear Materials likiwa na barabara ilijengwa kisasa na yenye haiba nzuri, barabara hiyo na eneo hilo litawekwa vivutio na upandwaji wa miti ya bustani inayolingana na minazi ili kuvutia zaidi kwa kushirikiana na wadau watakaopendekezwa kushiriki kutekeleza kampeni hii.

## MALENGO YA KAMPENI

- Kusafisha maeneo ya wazi, masokoni, hospitali na vituo vya afya, maskuli na mitaa ndani ya Wilaya ya Kati.
- Kuweka na kutunza bustani za kijani.
- Kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya nishati safi kama majiko bunifu na gesi safi ya kupikia.
- Kujenga uwezo kwa jamii kushiriki katika utunzaji wa mazingira.
- Kuwa na majukwaa na Vilabu hai vya usafi na mazingira katika kila Wadi na Shehia zake.

## SHUGHULI KUU ZA KAMPENI

- ✓ Usafi wa maeneo ya umma (masoko, barabara, Skuli, Hospitali).
- ✓ Upandaji miti na uanzishaji wa bustani za kijani.
- ✓ Warsha na semina kwa jamii juu ya nishati safi.
- ✓ Ugawaji wa vifaa vya usafi na majiko bunifu kwa kaya maskini.
- ✓ Uhamasishaji kupitia redio, mitandao ya kijamii na vipeperushi.
- ✓ Kufanya ukaguzi (inspection) wa siri kwa wafanyabiashara na mahoteli ili kutoa zawadi kwa watakaofanya vizuri kwenye usafi
- ✓ Kufanya ufunguzi na ufungaji wa kampeni

## WADAU MUHIMU

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kati

Masheha wa Wilaya ya Kati

Wananchi wa Wilaya ya Kati

Baraza la Mji Wilaya ya Kati (Watendaji na Madiwani)

Wakala wa Usafi na Mazingira (ZEMA) (Waatalamu wa Mazingira)

Wizara ya Maji, Nishati na Madini

Wakala wa Barabara

Taasisi za kiraia na mashirika ya maendeleo ya ndani ya Wilaya ya Kati

Wamiliki wa Mahoteli za Wilaya ya Kati

Wafanya biashara wa Wilaya ya Kati

Vikundi vya kijamii na NGO's (ZAVECO) ndani ya Wilaya ya Kati

## MAKADIRIO YA BAJETI YA KAMPENI KWA KIPINDI CHA MIEZI 6

| SHUGHULI | MAHITAJI | GHARAMA (TZS) |
|---|---|---|
| Ununuzi wa vifaa vya usafi | Mifagio, ndoo, gloves, dustbins (50*100,000/=) n.k | 4,000,000 |
| Mafunzo ya nishati safi | Warsha 2 | 3,000,000 |
| Upandaji miti na bustani | Miche 1000<br>Maji ya kunywa kwa washiriki<br>Uangalizi na usimamizi wa zoezi | 3,500,000 |
| Ufunguzi wa Kampeni | Washiriki 1000<br>Maji<br>Viti na Ukumbi<br>Vipaza sauti<br>Vipeperushi | (2,967,500)<br>467,500<br>?<br>200,000<br>300,000 |

| | | |
|---|---|---|
| | T – shirts na kofia 1000 | 2,000,000 |
| Ushirikishaji jamii (media + vipeperushi) | Vipindi vya Redio 2 na TV 2<br>Mabango<br>Vipeperushi | 2,500,000 |
| Ugawaji wa majiko bunifu | Kaya 100 | 5,000,000 |
| Ufatiliaji na Tathmini | Ripoti za maendeleo ya kampeni<br>Watu 6 kwa miezi 6 | 6,000,000 |
| Usafiri na mafuta kwa shughuli | Gari + mafuta lita (1,000) | 3,000,000 |
| T-shirts na Kofia | Kofia 300 na flana 500 | 8,000,000 |
| Kufunga Kampeni na kutoa Tunzo | Vipaza sauti<br>Viti<br>Ukumbi/uwanja<br>Waandishi wa habari<br>Maji<br>T-shirts na Kofia 2000<br>Bracelets 300<br>Washiriki | 200,000<br>1000,000<br>?<br>200,000<br>900,000<br>15,000,000<br>1,500,000<br>(18,600,000) |
| Cadres/volunteers (motivation) | 20 volunteers x miezi 6 | 3,000,000 |
| Fedha ya dharura | - | 432,500 |
| **Jumla** | | **63,000,000/=** |

## VIASHIRIA VYA MAFANIKIO (Indicators)

Ongezeko la usafi katika maeneo yaliyolengwa.

Idadi ya kaya zinazotumia nishati safi kuongezeka.

Idadi ya kaya zinazotumia vyoo rasmi

Ushiriki wa jamii katika usafi na utunzaji wa mazingira.

Upandaji wa miti kufanikishwa kwa kiwango cha 90% ya malengo.

## HITIMISHO

Kampeni hii inaleta mabadiliko chanya kwa mazingira na maisha ya wakazi wa Wilaya ya Kati. Ushirikiano kati ya taasisi za Serikali, jamii na sekta binafsi ni muhimu kufanikisha utekelezaji wa kampeni hii, sambamba na sera na mikakati ya maendeleo ya kitaifa na kikanda iliyopo.

| SN | SHUGHULI KUU KAMPENI | SHUGHULI NDOGO*2 | ENEO HUSIKA | MAHITAJI | MUDA | WAHUSIKA NA MAHITAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Usafi wa maeneo ya umma (Hoteli, Skuli, Hospitali, Masoko, Barabara, Nyumba, Usafiri wa Umma na binafsi) na Vyuo vikuu | Kutoa elimu<br>Kuweka Dustbins<br>Kusafisha maeneo | Pr.&Sec Dunga School, Miwani, Chwaka, Kijibwe mtu, Ghana, Kibele, Charawe, Uzi Ng'ambwa. | Maji ya kunywa, Usafiri<br>Mafyagio ya njukuti<br>Mabero, Mask, Gloves, Slesha, Mapanga, Majembe, dustbins Waandishi wa habari, Vipeperushi | 7-8/2025 | Watendaji wa BMK na Wilaya, Masheha na wajumbe, Wananchi wao, Wanafunzi na walimu Waziri wa Elimu, |
| | | | Ukongoroni, Tunguu, Uroa (Afya, fukwe na Hoteli), Mpapa, Uzini, Machui, Mwera Pongwe, Uzi | Maji ya kunywa, Usafiri<br>Mafyagio ya Kunjukuti<br>Mabero, Mask, Gloves, Slesha, Mapanga, Majembe, Waandishi wa habari, Vipeperushi | 7-8/2025 | Watendaji wa BMKna Wilaya, Masheha na wajumbe, Wananchi wao, Wanafunzi na walimu Waziri wa Elimu, vikundi vya michezo, Vikundi vya usafi, Makundi ya vijana na Chama na JKU |
| | | | Chwaka hoteli na Chuo, Kikungwi | ‘’ | 7-8/2025 | ‘’ |
| | | | Soko la Chwaka, Kikungwi, | ” | 7-8/2025 | |
| | | | Dunga Mitini-Kibaoni, Mwera Pongwe, Koani via Machui, Mchangani Shamba, Umbuji, Chwaka Kituo cha Polisi | ” | 7-8/2025 | |
| | | | Nyumba za Mpapa, Kiboje Mkwajuni, Kidimni road, Ofisi zote za Wilaya, Jumbi juu ya Kilima, | | 7-8/2025 | |
| | | | SUZA, IPA na ZU | | 7-8/2025 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Upandaji miti na uanzishaji wa bustani za kijani na Uzinduzi wa Kampeni | **Upandaji wa miti**<br><br>(maeneo ya barabara, sehemu za fukwe, Skuli, Vituo vya Afya,)<br><br>(Palm tree, Mikoko, Miti ya Matunda) | Tunguu (bango la mkoa mpaka tunguu (round)<br><br>dunga (mwera mitini mpaka tunguu round),dunga zuze.<br><br>Chwaka (kibaoni mpaka chuo cha fedha) | Gari la maji,mbolea,maji,miche,vifaa vya kuchimba (sururu, jembe, pauro, bero, wafanyakazi wa mawasiliano na waandishi wa habari.<br><br>Mtaalamu wa mimea. | 9 -10/2025 | Watendaji wa BMK na Wilaya, Masheha na wajumbe, Wananchi, wafanyakazi wa mawasiliano. |
| | | | Tunguu( Skuli ya jumbi msingi) Skuli ya Marumbi msingi na Mwera msingi | Mbolea, maji, miche, vifaa vya kuchimba (sururu, jembe, pauro, bero, wafanyakazi wa mawasiliano na waandishi wa habari.<br><br>Mtaalamu wa mimea. | 9 -10/2025 | Watendaji wa BMK na Wilaya, Afisa Elimu wilaya,walimu na wanafunzi,masheha, wananchi |
| | | **Upandaji wa bustan** | Vituo vya daladala (hanyegwa mchana, jumbi kwa bimdau,tunguu mahakamani,suza,) | Miche ya bustani, mbolea,gari la kumwagilia maji,dawa za kuulia wadudu,sprayer, | 9 -10/2025 | Watendaji wa BMK na Mkoa,wanafunzi wa chuo,masheha ,wananchi na vikundi vya ccm. |
| | | | Taasisi za Serikali (Ofisi ya BMK, Mkuu Wilaya, na Kilimo. | Miche ya bustani, mbolea, mipira, keni, ,dawa za kuulia wadudu,sprayer, | 9 -10/2025 | Watendaji wa BMK, kilimo na Wialaya, |
| | | | Vituo vya Afya<br><br>(dunga,Uroa na tunguu) | Bustani za maua na miche tiba, maji na usafiri. | 9 -10/2025 | Watendaji wa BMK na watemndaji wa ofisi wilaya (DHMT) DMO, sheha na wajumbe |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Warsha na semina kwa jamii juu ya nishati safi. | Kutoa elimu juu ya umuhimu wa matumizi ya nishati safi. | Shehia (Ghana,miwani,mwera kichaka mabundi, kibele,unguja ukuu kaebona,charawe,umbuji,chwaka) | Ukumbi,Wakufunzi(mamlaka ya mazingira, Zura), maji,chakula note book, peni , kwa wakufunzi,,projector, kifaa cha nishati safi,( gas),viperurushi. | 9 -10/2025 | Kamati, masheha,na wananchi wa shehia.na wakufunzi, Mkuu wa Mkoa |
| 4 | Ugawaji wa vifaa vya usafi na majiko bunifu kwa kaya maskini. | Kugawa vifaa vya usafi na majiko bunifu (fyagio,reki slesha na dawa za kusafishia choo). | Shehia (Kiboje ,kijibwemtu,chwaka kaskazi,miwani,dunga njia4, ukongoroni , binguni, na U/ukuu tindini. | Usafiri,,vifaa( fyagio,reki,slesha,na dawa za kusafisha choo,maji,)na majiko bunifu (mitungi ya gesi,majiko ya nishati ya jua. | 11-12/2025 | Kamati,Sheha,wananachi na Mgeni rasmi( Mkurugenzi BMK) |
| 5 | kupitia redio, mitandao ya kijamii na vipeperushi. | Kutoa elimu juu ya utunzaji na uhamasishaji wa mazingira. | Redio (ZBC na Kati fm),facebook,tiktok,Instagram,You tube ,vipeperushi | waaandisi wa habari2,(zbc na kati fm), Afisa Uhusiano na Habari BMK), | 11-12/2025 | waaandisi wa habari2,(zbc na kati fm), Afisa Uhusiano na Habari BMK),Mtendaji Bmk (1) |
| 6 | Kufanya ukaguzi (assessment) wa siri kwa wafanyabiashara na kutoa zawadi kwa ambae atakuwa anadumisha usafi. Na kufunga Kampeni | | Sheia zote za wilaya ya kati. | Usafiri,Askari, watendaji wa BMK,(afisa mazingira) | 12– 1/2026 | Afisa mazingira, muandishi wa habarI ,afisa uhusiano,mkurugenzi BMK. |